Andiko la Kisera, Oktoba 2021

# Kwa nini Ulipiaji Huduma za Maji ni Muhimu kwa Uhifadhi Madhubuti wa Milima ya Tao la Mashariki Nchini Tanzania?

## Ujumbe Muhimu

- Wazo la Ulipiaji wa Huduma za Mfumoikolojia (yaani Payment for Ecosystem Services) lina nafasi kubwa ya kuleta motisha kwa wasimamizi na wamiliki wa misitu katika kuimarisha shughuli za uhifadhi.
- Ulipiaji wa huduma za maji unaweza kuwa ni chanzo muhimu cha fedha kinachoweza kujazia bajeti ya serikali inayotengwa kwa ajili ya usimamizi wa sekta ya msitu.
- Huduma za maji zinalipiwa kwa namna moja ama nyingine, hata hivyo hakuna mfumo maalumu unaowezesha ugawanyaji wa mapato yanayotokana na ulipiaji huo kurejeshwa na kwenda moja kwa moja katika shughuli ambazo zingesaidia kuimarisha uhifadhi wa vyanzo vya maji.
- Uwepo wa Mfuko wa Uhifadhi wa Milima ya Tao la Mashariki (EAMCEF) kama mfumo wa ufadhili, pamoja na uzoefu wake katika utafutaji na utoaji wa ruzuku kwa ajili shughuli za uhifadhi, ni fursa muhimu ya skuelekeza malipo ya huduma za Mfumoikolojia kwa ajili ya uhifadhi wa Milima ya Tao la Mashariki.

## 1. Utangulizi

**Ulipiaji wa Huduma za Mfumoikolojia (Payment for Ecosystem Services) kwa ujumla wake humaanisha uwepo wa skimu inayohusisha kuwalipa wamiliki wa ardhi au maliaisili fulani kwa sababu ya huduma inayotolewa na ardhi au maliasili husika, malipo hayo yakiwa ni gharama ambayo ingelipwa ikiwa huduma hiyo isingekuwepo.**

Ripoti ya ya uchambuzi ya Millenium Ecosystem ya mwaka 2005 imefafanua Huduma za Mfumoikolojia kuwa ni manufaa wanayojipata watu kutoka katika mfumoikolojia ikijumuisha huduma za moja kwa moja kama vile chakula na maji, huduma za udhibiti kama vile udhibiti wa mafuriko na. magonjwa, huduma za kiutamaduni kama vile manufaa ya kiimani na huduma za vivutio na huduma saidizi kama vile uwezeshaji wa mzunguko wa virutubishi. Huduma hizi huwezesha uwiano wa maisha katika dunia.

Kupitia tafiti mbalimbali zilizofadhiliwa na Mfuko wa Uhifadhi wa Milima ya Tao la Mashariki (EAMCEF) na washirika wengine, huduma muhimu za mfumoikolojia wa Milima ya Tao la Mashariki zilibainishwa na jumla ya thamani zake kiuchumi zilikadiriwa. Huduma hizi ziliwekwa katika makundi ya mazao ya kilimo, rasilimali za maji, bidhaa za misitu zilizovunwa, bioanuwai, miti ya mbao, utalii, thamani ya uwepo wa mfumo huo, huduma ya ufyonzaji wa kaboni, udhibiti wa mafuriko na mmomonyoko wa udongo. Kwa namna hii, Ulipiaji wa Huduma za Mfumoikolojia ungemaanisha kuweka kwa utaratibu madhubuti ambapo baadhi ya huduma muhimu zinazotolewa na mfumoikolojia (ambazo nyingi hazijabainishwa katika bei za masoko) zitalipwa kama fidia ili kuwaruhusu wamiliki na wasimamizi kuimarisha upatikanaji wa huduma hizo na/au kufidia gharama za kutokuyatumia maeneo hayo kwa shughuli nyinginezo, isipokuwa kuyahifadhi na kuyatunza ili kuhakikisha upatikanaji wa huduma husika.

Andiko hili halilengi kuongelea huduma zote za mfumoikolojia zinazotolewa na Milima ya Tao la Mashariki bali linajikita katika huduma za maji pekee kutokana na athari zake za moja kwa moja katika shughuli kuu za kiuchumi nchini na pia kwa ajili ya kufafanua kwa urahisi wa wazo la Ulipiaji wa Huduma za Mfumoikolojia.

**Andiko hili linajibu maswali makuu matatu: Kwa nini kulipia, nani anapaswa kulipa na nani anapaswa kulipwa kwa huduma za maji?**

## 2. Misitu ya Milima ya Tao la Mashariki ni maeneo ya vyanzo vya maji

Milima ya Tao la Mashariki imesambaa kutoka kusini mwa Tanzania mpaka kusini Mashariki mwa Kenya ikiwa na ukubwa wa eneo la bloku za milima linalofikia kilometa za mraba 23,000, bloku hizi huunda umbo umbo kama la upinde na hivyo kufanya safu hizi. Milima ya Tao la Mashariki inaundwa na bloku 13 za milima ya Upare Kasikazini na Kusini, Usambara Magharibi na Mashariki, Nguu, Nguru, Ukaguru, Uluguru, Malundwe, Rubeho, Udzungwa na Mahenge kwa upande wa Tanzania pamoja na vilima vya Taita nchini Kenya. Bloku 12 kati ya hizo zipo upande wa Tanzania. Kwa upande wa Tanzania bloku za milima zimeenea katika zaidi ya wilaya 15 zilizo katika mikoa mitano ya Tanzania ambayo ni Tanga, Kilimanjaro, Morogoro, Dodoma na Iringa

Milima ya Tao la Mashariki imesheheni misitu ya mvua na ardhi yenye nyasi. Misitu ya milima hii ni maeneo muhimu ya vyanzo vya maji. Kwa kuwa vyanzo vya maji, misitu hii hukusanya maji ya mvua na maji yanayotiririka na kuyaelekeza katika mito, mabwawa, maziwa au mfumo wa maji ya ardhini hivyo kudhibiti utiririkaji wa maji katika mfumoikolojia kwa wakati wote. Maji kama huduma muhimu ya mazingira ni muhimu kwa ajili

ya uendelevu wa biaoanuwai zilizopo na kwa shughuli za binadamu. Mito inayotoka katika Milima ya Tao la Mashariki hutegemewa na takribani 25% ya Watanzania. Mito mingi ya upande wa Mashariki mwa Tanzania hujipatia maji yake kutoka katika vyanzo vilivyoko katika Milima ya Tao la Mashariki. Milima hii ni vyanzo vya maji yanayotumika kuzalisha umeme,, shughuli za kilimo cha mazao ya chakula na mazao ya biashara (kwa mfano, mpunga, mahindi, miwa, mazao ya misitu, chai, kahawa n.k.), matumizi ya nyumbani na viwandani. Miji na majiji yanayozunguka Milima ya Tao la Mashariki kama vile Dodoma, Iringa, Tanga, Dar-es-Salaam, Morogoro, Ifakara, Lushoto, Mwanga, Same, Mombo, Korogwe, Soni, Kilosa, Muheza, Kibaha, Mpwapwa, Mvomero, Turiani, Kilindi, Gairo, Mikumi, Chalinze, Handeni na Kilolo hutegemea maji ambayo vyanzo vyake vipo katika Milima ya Tao la Mashariki. Mito mikuu inayoanzia katika vyanzo hivi ni pamoja na Mto Ruvu, Mto Zigi, Mto Wami, Mto Kilombero, Mto mdogo wa Ruaha na Mto Pangani.

Kwa upande wa umeme, jumla ya thamani ya kiuchumi ya umeme unaotokana na maji kutoka katika mfumoikolojia wa Milima ya Tao la Mashariki inakadiriwa kuwa sawa na Dola za Marekani bilioni 66 ambayo ni sawa na 28% ya jumla ya thamani ya kiuchumi ya mfumoikolojia wote. Milima ya Tao la Mashariki ni chanzo kikuu cha zaidi ya 90% ya umeme unaotokana na maji unaozalishwa katika vituo vikuu vya Kidatu, Mtera, Kihansi, Maporomoko ya Pangani na kituo cha kuzalisha umeme cha Hale na Bwawa la Nyumba ya Mungu. Pia, kituo cha kuzalisha umeme cha Julius Nyerere kinategemea maji kutoka Milima ya Tao la Mashariki.

## 3. Kwa nini kulipia, nani alipie, na mlipwaji ni nani kwa huduma za maji?

Kwa nini ni muhimu kulipia, nani anapaswa kulipia na nani anapaswa kulipwa? Haya ni maswali makuu matatu ambayo andiko hili linatoa majibu. Maji ni rasilimali inayopatikana kiasilia na kwamba huwa siku zote huwa katika mzunguko endelevu katika dunia na angahewa. Katika mzunguko huu wa maji, misitu ya Milima ya Tao la Mashariki huwa ni la eneo muhimu katika kuyapokea maji (kama ilivyokwishaelezwa katika sehemu iliyotangulia) na hivyo kuzalisha mito ya maji. Kutokana na umuhimu wa misitu hii kuwa ni vyanzo vya maji, serikali ya Tanzania ilitenga maeneo muhimu ya Milima ya Tao la Mashariki kuwa ni Maeneo ya Hifadhi yanayopewa kipaumbele na hivyo kuweka jitihada katika kushughulikia vyanzo vikuu vya ukataji miti ovyo na uharibifu wa misitu ili kuakikisha kuwa huduma za upatikanaji wa maji zinakuwa endelevu. Licha ya kukabiliwa na ufinyu wa fedha zinazotengwa katika bajeti ya serikali, mamlaka zinazohusikana maeneo haya zimekuwa zikichukua hatua stahiki ili kulinda maeneo muhimu.

Kwa sasa watumiaji wakubwa wa maji tayari wanalipia huduma za maji kwa namna moja ama nyingine, hata hivyo haijulikani ni kwa kiasi gani sehemu ya malipo hayo hurejeshwa katika kusaidia wasimamizi wa misitu. Andiko hili linatoa msisitizo juu ya umuhimu wa kuweka mfumo madhubuti ambapo watumiaji wakubwa wa maji na watumiaji wengine watachangia katika usimamizi wa maeneo ya vyanzo vya maji kupitia utaratibu wa ulipiaji wa huduma za maji. Kwa mfano, katika utaratibu uliopo sasa, watumiaji wa maji wa majumbani hulipia kila mwezi ankara zao za matumizi ya maji (zinazokokotolewa kwa kuzingatia kiasi kilichotumika) kwa Mamlaka za Maji, lakini haijulikani ni kiasi gani cha mapato hayo hutengwa kwa ajili ya kusaidia uhifadhi wa vyanzo vya maji. Makampuni binafsi ya biashara hutumia maji katika viwanda vyao na kujipatia faida kutokana na bidhaa zao lakini haijulikani ni kwa kiasi gani makampuni haya huchangia katika shughuli za uhifadhi wa vyanzo hivyo vya maji. Kuna haja ya kuwa na Mfumo Madhubuti ili kuwaongoza watumiaji wakubwa wa maji, kwa hiari yao, kulipia kikamilifu huduma za maji na kuhakikisha kuwa kiasi fulani kinatengwa ili kusaidia uhifadhi wa vyanzo vya maji. Uwepo wa mfumo maalumu utasaidia katika kuweka mwongozo wa namna ambayo malipo hayo ya maji yanaweza kupenyezwa na kuwafikia wanajamii wanaoshirikiana na serikali katika uhifadhi wa misitu.

## Kuhusu Mfuko wa Uhifadhi ya Milima ya Tao la Masharikі (EAMCEF)

Mfuko wa Uhifadhi wa Milima ya Tao la Mashariki (EAMCEF) ni Mfuko wa udhamini ulioanzishwa na unaofanya kazi kama mkakati wa muda mrefu na wa uhakika wa ufadhili wa shughuli za maendeleo ya jamii, tafiti za uhifadhi na kuendeleza bioanuwai, huduma za kiikolojia na matumizi endelevu ya maliasili katika Milima ya Tao la Mashariki iliyoko nchini Tanzania. EAMCEF hufanya kazi kama asasi isiyo ya Serikali isiyo ya Biashara, hutafuta fedha na hutoa ruzuku kwa Idara za Serikali (serikali kuu na serikali za mitaa), Asasi Zisizo za Serikali, Wanajamii, Taasisi za Utafiti, Taasisi za Elimu, Kampuni Binafsi pamoja na watu binafsi

**Kwa taarifa zaidi tafadhali wasiliana na:**


**Sekretarieti ya EAMCEF,**
Kiwanja Na. 348, Eneo la Forest Hill, Barabara ya Kingalu,
S.L.P. 6053, Morogoro, Tanzania.
Simu ya Mezani: +255 (0) 23 2934274.
Simu ya Mkononi: +255 (0) 755 330558.

**Barua Pepe:** eamcef@easternarc.or.tz.
**Tovuti:** www.easternarc.or.tz
**Twitter:** www.twitter.com/eamceftanzania
**Instagram:** www.instagram.com/eamceftanzania
**Facebook:** www.facebook.com/eamcef